



## “TOHARA KWA WANAUME: KUPIMA FAIDA NA HASARA”

Tohara kwa wanaume ni oparesheni inayohusu kuondolewa kwa sehemu ya ngozi au ngozi yote inayofunika kichwa cha uume, na imekuwa ikifanywa na baadhi ya watu katika makabila na dini mbalimbali kwa zaidi ya maelfu ya miaka.

Kwa sasa tohara kwa wanaume imeamsha mvuto mkubwa wa kisayansi na uchunguzi kwa sababu utafiti umethibitisha kuwa **wanaume waliotahiriwa wana viwango vidogo vya maambukizo ya VVU** kuliko wasiotahiriwa. Aidha ueneaji wa VVU ni mdogo kwa jumla katika jamii zinazotahiri wanaume kuliko zile ambazo wanaume hawatahiriwi.

Kiasi cha asilimia 20 cha wanaume duniani kote inasemekana kuwa wametahiriwa, iwe mara baada ya kuzaliwa au wakati wa balehe, kwa kawaida kutokana na sababu za kiutamaduni, kiafya au dini. Si nchi zote Barani Afrika zenye takwimu, kuhusu ushauri wa tohara kwa wanaume, hata hivyo kwa kawaida inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 20 ya wanaume kusini mwa Jangwa la Sahara wametahiriwa, kati ya asilimia 50 na 80 katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki, na zaidi ya asilimia 80 au zaidi katika Bara la Afrika.

### Kinachofahamika ni Nini?

Utafiti wa majaribio wa mara ya tatu Afrika Mashariki na Kusini ambao umefanywa, miaka ya hivi karibuni kupima kwa njia ya utafiti uliodhibitiwa, manufaa ya tohara kwa wanaume katika kuzuia maambukizi ya VVU. Utafiti uliofanywa katika Jimbo la Gauteng, Afrika Kusini, ulisimamishwa mapema zaidi kuliko ulivyopangwa kwa sababu matokeo yamethibitisha kuwa tohara ilikuwa kinga dhidi ya maambukizi ya VVU na wachunguzi wamependekeza kuwa utaratibu huo uendelee kwa watu zaidi ya 3,274 wanaoshiriki.

- Wanaume waliotahiriwa waliofanyiwa utafiti wameonekana kuwa ni asilimia 60 pungufu ya uwezekano wa kuambukizwa VVU kuliko wasiotahiriwa.
- Iwapo utafiti wa majaribio unaoendelea nchini Kenya na Uganda unaowahusisha wanaume 8,000 utatoa matokeo sawa na yale ya Afrika Kusini, tohara kwa wanaume itaungana na zana kama vile Kondomu za kiume na za kike kama njia kuu za kuzuia maambukizi ya VVU.
- Tayari msingi wa shauku umeonekana nchini Botswana na Swaziland, nchi mbili miongoni mwa nchi zilizoathiriwa sana na VVU/UKIMWI.
- Zaidi ya asilimia 80 ya wanaume waliofanyiwa utafiti Botswana wamesema kuwa wangependa kutahiriwa iwapo utaratibu huo ni salama na wenye gharama nafuu.
- Nchini Swaziland zile hospitali ambazo hazikuwa zikitahiri, sasa zimekuwa zikitahiri watu 10-15 kwa juma na zina orodha ndefu ya watu wanaosubiri huduma hiyo.



# TAARIFA HALISI NAMBA SABA



Hivi sasa mjadala unaendelea katika jamii ya Waswazi ambayo kwa kawaida haitahiri wavulana wakati wowote, wakati wengine wanalaumu utaratibu huo kama ni kosa, katika mila na desturi za Waswazi, wengine wanadai kuwa Serikali iendeleze tohara kama sehemu ya Sera ya afya ya umma.

## Uchunguzi Unaowiana

Hata hivyo, ingawa inaweza kuthibitishwa kuwa inachangia kinga, **tohara kwa wanaume bado haiwezi kuitwa sindano ya miujiza**. Katika nchi za Afrika Magharibi ambako kwa kawaida wanaume wanatahiriwa, maambukizi ya VVU yanazidi kuenea.

Aidha masuala yafuatayo yanaleta wasiwasi wa kweli:

- Katika maeneo ambayo hayana huduma za afya, wanaume wenye shauku ya kujilinda wanaweza kufanya tohara katika mazingira na vifaa visivyotakaswa vizuri, na/au tohara inaweza kufanywa na watu wasio na ujuzi wala mafunzo.
- Wanaume wanaweza kukosea kuamini kwamba mara wanapotahiriwa, basi wamekingwa kwa ukamilifu dhidi ya VVU, na hivyo kuacha kutumia Kondomu.
- Wakati wa kipindi cha kupona (kiasi cha mwezi mmoja baada ya tohara) kwa kawaida wanaume wako hatarini zaidi kuambukizwa VVU.
- Hoja hizi zinadhihirisha kwamba iwapo tohara inathibitishwa kuwakinga wanaume na maambukizo ya VVU, inahitajika kuonekana kuwa ni kipengele kimoja kati ya mkakati kabambe wa kinga utakaojumuisha: matumizi ya kila mara ya Kondomu, mabadiliko ya tabia, upimaji wa hiari na ushauri nasaha.
- Kutokana na shauku kubwa ya tohara kufuatia matokeo ya majaribio ya Afrika Kusini, Serikali hazina budi kuchukua hatua madhubuti mapema ili kuhakikisha kuwa, tohara kwa wanaume inafanywa na watu wenye mafunzo, katika mazingira salama na yenye vifaa vya kutosha; ili kupunguza uwezekano wa kutokea matatizo. Iwapo itafanywa ipasavyo, katika mazingira yanayofaa na yaliyotakasishwa, kiwango cha matatizo baada ya tohara ni kidogo sana, yaani asilimia 0.2 hadi 2 tu.